**SCENE 1**

**EXT. SHEKUWE'S MANSION. GATE. DAY (2)**

**BE CHARO. MOMO. BITOTO**

BE CHARO ANASINZIA GETINI, GHALFA ANAGUTUSHWA NA MLIO WA HONI GETINI. ANAENUKUA NA KUCHUNGULIA. ANAPOJUA NI NANI, ANACHANGAMKA KUFUNGUA GETI. GARI LINAINGIA NDANI. BE CHARO ANAHARAKISHA KUFUNGA GETI. MOMO NA BITOTO WANASHUKA GARINI. BE CHARO ANAKUJA MBIO KUMLAKI MOMO!

**BE CHARO**

*(Akionekana mwenye furaha tele)* Mamaaa! Mama! Ni wewe au naota?

**MOMO**

*(Akitabasamu)* Ndoto zako huwa zanukia al oud?

**BE CHARO**

Aaah hamna hata nikaota niko Jeddah! Karibuni.

**MOMO**

Asante! Muite TUMU aje akusaidie mizigo...

**BE CHARO**

Mama hamna TUMU tena, muna tamu la WARIDI... *(Amuashiria kwa jicho)*

WARIDI ATOKA NDANI. MOMO NA BITOTO WANAMUANGALIA ANAVYOTEMBEA KWA MADAHA, NGUO YAKE YA KAZI IKIONEKANA FUPI ZAIDI.

**WARIDI**

*(Anawaamkua na kuinamisha magoti chini kidogo kama ishara ya heshima)* Habari za asubuhi!

**MOMO**

*(Anatabasamu na kumuiga alivyowasalimia)* Tushaziona! Hebu msaidie mwenzako kutoa mabegi! *(Anawapiata, wanageuka na kumuangalia)*

**BITOTO**

Dadangu, huyu ni kijakazi au ndiyo umeletewa wa tatu?

**MOMO**

Alete hata arubaini watatoka wote! *(Wanaingia ndani)*

PAN: to

LEILA AKIWA JUU DIRISHANI, ANATOKA DIRISHANI MBIO. SADA NA SULTAN WANASIMAMA JUU KIBARAZANI NA KUWAANGALIA.

**SADA**

Jana tuliambiwa nyani yuwaja kumbe alikuwa aje na mtoto wake?

**SULTAN**

Mtoto ama jitoto? Maa mdogo, hapa itabidi tuombe serikali vitoa machozi, nishaona vita vya masugu!

**SADA**

Hawa wasikubabaishe, hata wakajileta kama mawimbi, kisha watatulia!

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SCENE 2**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. ASHA'S BEDROOM. DAY**

**LEILA. ASHA. SHEKUWE**

LEILA ANABISHA MLANGO WA ASHA KWA VISHINDO HUKU AKIONEKANA MCHANGAMFU.

**LEILA**

Baba! baba! Baba amka!

MLANGO UNAFUNGULIWA NUSU NA FURAHA ILIOKO USONI MWAKE INAPOTEA ANAPOMUONA ASHA AMESIMAMA MLANGONI, BADO AKIWA AMEVALIA MAVAZI YAKE YA KULALA.

**LEILA**

*(Anachungulia ndani)* Baba ashaamkai?

**ASHA**

Leila, tabia gani hizo kubishia watu alfajiri tena kwa vishindo kisha hata salamu huna.

**LEILA**

Za asubuhi? Baba yu wapi?

**ASHA**

Amelala! Kuna nini?

**SHEKUWE**

*(Anatokeza kwa nyuma)* Leila una nini, mbona unakera watu asubuhi...

**LEILA**

*(Anatabasamu)* ...mama ashakuja! Yuko chini!

**SHEKUWE**

Sawa, nenda, naja!

LEILA ANASHUKA CHINI MBIO. ASHA ANARUDI NDANI NA KUKETI KITANDANI. SHEKUWE ANAMUANGALIA NA KUHISI BADO HAJAFURAHISHWA NA HABARI HIZO.

©Ibrahim Chitayi © Maina Denis Wanjohi

**SHEKUWE**

Naona ungejitayarishe, tushuke pamoja tukamkaribishe mwenzako.

**ASHA**

Mwenzako niko naye tumboni. Wewe nenda.

SHEKUWE ANASHINDWA KUMJIBU. ANACHUKUA KANZO YAKE NA KUIVAA KWA JUU. ASHA ANAMUANGALIA AKITOKA. HANA RAHA.

**SCENE 3**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY (D2)**

**MOMO. LEILA. BITOTO. SHEKUWE**

LEILA ANATOKEZA NA KUMKUMBATIA MAMAKE HADI MOMO ANASHANGAZWA NAYE.

**MOMO**

Ah Leila polepole basi usije ukaniangusha!

**LEILA**

Mama hujui nilivyokutamani. Shikamoo!

**MOMO**

Marahaba kipenzi changu! *(Kwa Bitoto)* Mbona humuamkui mamako mdogo, au umemsahau?

**LEILA**

Aaaah maa Bitoto, kwa nini nimsahahu, shikamoo!

**BITOTO**

Marahaba mwanangu! *(Anamuangalia alivyojisongeza kwa Momo)* Mtu na mamake huwezi watenganisha hata kwa dawa! *(Wanacheka)*

**MOMO**

Vipi, babako yuko wapi?

KABLA LEILA HAJAJIBU, SHEKUWE ANATOKEZA, WANAANGALIANA NA MOMO KWA MDA. LEILA ANATAZAMA CHINI. BITOTO ANAPESA PESA MACHO HATAKI KUMUANGALIA SHEKUWE MACHONI.

**SCENE 4**

**INT. LENOX'S HOUSE. BEDROOM. DAY (d2)**

**LENOX. DORA**

DORA AMEKETI KITANDANI, MIGUU YAKE IKINING'INIA CHINI. LENOX AMEKETI CHINI KABISA. MBELE YAKE MNA BESENI LA MAJI MOTO, MAFUTA YA NAZI KWA KANDO NA AMESHIKILIA KITAMBARA. ANAKITIA KILE KITAMBARA MAJI NA KUUSHIKA MGUU MMOJA DORA, ANAANZA KUUFUTA NA KILE KITAMBARA. DORA ANASOGEZA MGUU WAKE KANDO, KWA WOGA.

**DORA**

Ah Lenox utanichoma!

**LENOX**

Nitakuchoma vipi na maji hata si moto!

**DORA**

Weka uso wako humo ndani kama si moto!

**LENOX**

*(Anagusa na mkono wake)* Si moto mpenzi! Na je ningekuwekea maji baridi, ungeteta pia.

**DORA**

Siteti mpenzi, nasema tu! *(Anauregesha mguu wake)* Haya, lakini kamua hicho kitambara, usinichubue miguu nikashindwa kutembea.

**LENOX**

*(Anacheka)* DORA muoga sana wewe!

**DORA**

Si uwoga, ni mwili huu, si chuma!

**LENOX**

Au umetosheka niwache!

**DORA**

Hayo ni maneno yako, endelea hapo! *(Wanaangaliana na kucheka wote, kimya)* Jana nilikutana na Asha.

**LENOX**

Anaendeleaje?

**DORA**

Hana neno, anahesabu miezi tu, karibu atajifungua!

**LENOX**

Shekuwe anatamani ingekuwa kama leo hivi, angependa kuwa na mtoto wa kiume!

**DORA**

Kisha nimemwambia ASHA! Akakataa! *(Kimya)* La muhimu ni ile furaha nimeiona usoni mwa Asha. Imenifanya na mimi nika...wacha tu!

**LENOX**

Sema....unatamani mtoto?

**DORA**

Mtoto? Umri niliyofika itakuwa vigumu...

**LENOX**

Hata vinyanya huzaa sembuse wewe! Hujasikia *(Dora anacheka. Lenox anasimama na kuketi naye kitandani)* DORA! Bado hatujachelewa, tunaeeza kwenda kwa mtaalamu akatueleza zaidi kama inawezeka kupata mtoto au la!

DORA ANALALA KIFUANI MWA LENOX, LENOX ANAMSHIKA KAMA KULIWAZA.

**SCENE 5**

**INT. BEKA'S ONE BEDROOM APARTMENT. DAY (D1)**

**BEKA**

RUNINGA IKO WAZI. BEKA AMEKETI AKIELEKEA UPANDE WA RUNINGA ILA HATAZAMI, MAWAZO YAKE YAKO MBALI.

**SCENE 6**

**EXT/INT. ORPHANAGE. DAY/NIGHT - FLASHBACK**

**YOUNG BEKA. YOUNG MODDY. YOUNG BULLIES**

NB: MIXED LOCATIONS AND SCENERIOS INSIDE THE ORPHANAGE WHEN MODDY AND BEKA WERE YOUNG.

**UWANJANI**

VIJANA WANACHEZA MPIRA. BEKA MDOGO, NDIYO KIPA ILA HADAKI. ANAFUNGWA MABAO KARIBU YOTE. VIJANA WENZAKE WANAMFUATA NA KUMTISHIA HADI ANAANGUKA CHINI. MODDY MDOGO ANATOKEZA NA KUWATISHIA. WANATOKA MBIO. MODDY MDOGO ANAMPATIA BEKA MDOGO MKONO NA KUMUENUA. WANATABASAMU NA KUKUMBATIANA.

**SEHEMU YA MANKULI**

BEKA MDOGO AMEKETI MEZANI, WANAKUJA VIJANA NA KUANZA KUMSUMBUA, HUKU WAKIOKOTA CHAKULA CHAKE. MODDY MDOGO ANATOKA KWA MBELE NA KUWANG'ARISHIA. WANAREGESHA KILA WALICHOKICHUKUA KWENYE SAHANI YA BEKA MDOGO NA KUKIMBIA. BEKA MDOGO ANAMUANGALIA MODDY MDOGO NA KUTABSAMU.

**KWENYE MTI AU UKUTA**

AIDHA VIJANA WAMEMSHIKILIA BEKA MDOGO JUU CHINI WAKITAKA KUMUANGUSHA AU WAMEMFUNGA NA KAMBA MTINI. WANACHEKA. MODDY MDOGO ANATOKEZA.

FLIP IT.

MODDY MDOGO NA BEKA MDOGO WAMESIMAMA KWA CHINI WAKIMTAZAMA MMOJA YA WALE VIJANA. WAMEMFUNGA KWA KAMA MTINI AU WAMEWAAMURU VIJANA WENZAKE WAMESHIKILIE JUU CHINI. BEKA MDOGO NA MODDY MDOGO WANANGALIANA WAKICHEKA.

EDITOR: CONNECT YOUNG MODDY'S FACE WITH MODDY IN THE NEXT SCENE.

**SCENE 7**

**INT. MODDY'S BEDSITTER. DAY (D2)**

**MODDY**

MODDY AMELALA KITANDANI AKIPITIA NAMBA ZAKE, ANAPOFIKA KWA ASHA, ANASITA KIDOGO KISHA ANAPIGA. INALIA KWA MDA LAKINI HAISHIKWI. ANAKATA NA KUJARIBU TENA.

CUT TO:

**SCENE 8**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. ASHA'S BEDROOM. DAY**

**MODDY. ASHA**

ASHA AMEKETI KITANDANI, ANAITAZAMA SIMU YAKE IKILIA. ANAONA NI MODDY ILA ANASITA KUJIBU. INAPOZIDI KUITA NA KUANZA KUMKERA, ANAJIBU KWA HASIRA.

**ASHA**

Moddy wataka nini?

**MODDY V/O**

Aaah jamani, kwani salamu shilingi ngapi ninunue basi?

**ASHA**

Nilikwambia mimi ni mke wa mtu, unanipigia saa hizi ukitaka nini?

**MODDY V/O**

Naomba tukutane, nina mazungumzo muhimu na wewe... *(Kimya)* Hallo, Asha? Upo... *(Kimya)*Hallo? Asha!

MODDY ANAITAZAMA SIMU YAKE, BADO HAIJAKATIKA.

**MODDY V/O**

Asha? waniskia?

ASHA ANAWEKA SIMU YAKE KITANDANI NA KUIANGALIA HADI MODDY ANAKATA MWENYEWE.

**SCENE 9**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY**

**MOMO. LEILA. BITOTO. SULTAN. SHEKUWE. SHARIFU. SADA**

KIMYA. MOMO, BITOTO, LEILA WOTE WAMENYAMAZA WANAANGALIANA WAKITABASAMU KAMA AMBAYE WANAOGOPA KUONGEA.

**SHEKUWE**

Bitoto, nasikia siku hizi umegeuka mtalii. Hutulii nyumbani.

**BITOTO**

Shemegi hujui bila watalii uchumi utasimama!

**SADA**

*(Atokeza SULTAN akiwa nyuma yake)* Nawe wajua kusimamisha uchumi kweli mpaka bongo za watu! *(Anamvuta Sharifu, ambaye amejificha kwa kando)*

Mumeo Sharifu, amekutamani!

BITOTO ANAGUTUKA ANAPOMUONA SHARIFU. SHARIFU ANAPOMUONA BITOTO, ANAFYATUKA MBIO KAMA RISASI NA KUMKUMBATIA.

**SHARIFU**

Oooh mahabuba, nurulaini wa moyo wangu, chombo cha nafsi yangu...

**SADA**

*(Kwa Sultan)* ...si nilikwambia babako si chizi...mbona amemkumbuka mke wake?

KABLA SULTAN HAJAMJIBU SADA, SHARIFU ANAMSUKUMA BITOTO NA KUMUANGUSHA KOCHINI.

**SHARIFU**

Niondokee mwizi mkubwa wewe! Pesa zangu ziko wapi? Pesa zangu ziko wapi? *(Anataka kumshika)*

**SHEKUWE**

*(Anamshika)* Mzee Sharifu...tafadhali

**SHARIFU**

...Alaa nishawajua! Nyote gengi moja! Munataka kunidhulumu! Niwauzie nyumbani kisha muje muniibie pesa zangu! Leo Sharifu, mutanitambua!

SHARIFU ANAANZA KUMINYANA NA SHEKUWE. WOTE WANARUDI NYUMA KWA UWOGA. SHEKUWE ANAMSHIKILIA HADI ANATULIA. SHARIFU ANAMUANGALIA SHEKUWE.

**SHARIFU**

Baa mkwe, wajuwa kushikwa namna hii huwa sipendi! *(Shekuwe anamuachilia, Sharifu anajitengeza)* Mimi Sharifu bwana! Unafikiri wazee walipita hapa, wakuona umenikamata sampuli hii watasemaje! Tafadhali tuheshimiane.

SHEKUWE HASEMI KITU, WOTE WANASONGA KANDO NA KUMPISHA, SHARIFU ANATOKA KAMA BOSI KUBWA.

**LEILA**

Baba! Atakuja kutudunga visu siku moja.

**MOMO**

*(Anajifanya anahema)* Balaa gani mume wangu kutukaribisha na wendazimu! Ghafla nyumba imegeuka portrizi sijui ni mathare!

**ASHA**

*(Anatokeza)* Huyo mwendawazimu ana jina, anaitwa Mzee Sharifu, ni babangu, mume wa dadako. Na hapa ndiko anakoishi. Karibuni. *(Anatoka)*

WOTE WANABAKI KIMYA. BITOTO AKIONEKANA BADO AMEJAWA NA TAHARUKI.

**SCENE 10**

**EXT/INT. ORPHANAGE. GATE/COMPOUND. DAY (D2)**

**<u>BEKA. MAMA RUKIA</u>**

BEKA AMESIMAMA NJE YA GETI. ANAITAZAMA KWA MDA KABLA KUAMUA KUINGIA NDANI. USO WAKE UNAONYESHA AMECHANGANYIKIWA BADO HAJAFANYA UAMUZI. ANAPIGA HATUA KIDOGO KISHA ANARUDI NYUMA. GHAFLA ANASIKIA FUJO LA WATOTO. ANAPOCHUNGULIA ANAONA WATOTO WAKO NJE WANACHEZA. ANATABASAMU NA KUINGIA NDANI. ANASIKIA SAUTI YA MWANAMKE, NA ANAPOTAZAMA KWA KANDO, ANAMUONA MAMA MOJA UMRI WA 50s HIVI, ANAMUANGALIA AKITABASAMU.

**BEKA**

Mama RUKIA, shikamoo!

**MAMA RUKIA**

Marahaba! Mwanangu BEKA, leo umeamua kututembelea! *(Beka anatabasamu na kutazama chini)* Naona maisha yanakupeleka vizuri.

**BEKA**

Nashukuru mungu.

**MAMA RUKIA**

Naona bado pia hujasahau maadili tuliyokufunza.

**BEKA**

Siwezi.

**MAMA RUKIA**

Haya niambie, najua hukuja matembezi, sioni hata kifuko. *(Beka anatabasamu na kutazama chini kwa haya)*

**BEKA**

©Ibrahim Chitayi © Maina Denis Wanjohi

Nimeanza harakati ya kutafuta mamangu mzazi, sijui unaweza kunisaidia vipi?

**MAMA RUKIA**

Kusema kweli mwanangu, ningependa sana kukusaidia ila aliyekuleta hapa hatukumuona na hatumjui!

**BEKA**

Ki vipi?

**MAMA RUKIA**

Alikuwacha nje ya geti, na ulikuwa bado mwana mchanga!

**BEKA**

Hakuacha, karatasi yoyote, majina....

**MAMA RUKIA**

Tulikupata ndani ya kikapu, umefinikwa finikwa na shuka

BEKA ANAHISI KUKATA TAMAA, SICHO ALICHOTARAJIA.

**SCENE 11**

**INT. CITY MALL/MARINA. CAFE ARABIKA. DAY (D2)**

**MODDY. ASHA**

ASHA AMEKETI AKINYWA KAHAWA. MODDY ATOKEZA AKITAFUTA TAFUTA, ANAPOMUONA ANATABASAMA NA KUMFUATA KWA VISHINDO.

**MODDY**

Asha, wewe ndiyo wajua kuchagua maskani ya kukutana! *(Anaenama kumpatia busu)*

**ASHA**

*(Amzuia)* Keti! Na kwa taarifa yako huu mkahawa nimezoea kuja na mume wangu Shekuwe. Sio maskani ya kukutana mimi na wewe.

**MODDY**

*(Anamuangalia na kuketi)* Nimekuelewa! Hiyo mimba ndiyo yakutatiza.

**ASHA**

Inakutatiza wewe maanake huchoki kuitaja! Moddy, kipi muhimu ulichoniitia?

**MODDY**

Asha, nimekuwa nikiwaza kwa mda na singependa mtoto wangu apitie maisha yale me nilipitia

**ASHA**

Mtoto yupi?

**MODDY**

*(Acheka kidogo)* Bado unakuwa mgumu wa kukubali ukweli wa mambo.

**ASHA**

Ukweli gani Moddy? Una ushahidi gani huyu mtoto ni wako?

**MODDY**

Na wewe una uhakika gani ni wa Shekuwe?

**ASHA**

Kwa sababu nimekuwa naye kwa mda mwingi kukuliko wewe! Hisia zangu kama mamake huyu mtoto zinanielekeza kuwa babake ni Shekuwe.

**MODDY**

Kwa hivyo utaendelea na huo wazimu.

**ASHA**

Sio wazimu, ndiyo ukweli wa mambo, wataka ni hivyo, hutaki, zoea! *(Anaenuka na kuenda zake)*

**MODDY**

*(Anamuangalia akienda)* Tutazoea huyo mtoto akizaliwa.

©Ibrahim Chitayi © Maina Denis Wanjohi

**SCENE 12**

**INT. DOCTOR'S PLAZA. GYNECOLOGIST. DAY (D2)**

**DORA. DAKTARI**

DORA AMEKETI OFISINI MWA DAKTARI AKIONEKANA ANA WASIWASI. ANAFINYA FINYA VIDOLE VYAKE HUKU AKISUBIRIR. DAKTARI ANAINGIA HUKU AMEBEBA MAKARATASI KADHA, ANAYAPITIA NA KUKETI.

**DORA**

Daktari, majibu tayari? Samahani, usione nakuharakisha, ni vile nina hamu ya kujuwa kama inawezekana au la.

**DAKTARI**

Dora, ningependa unisikize kwa umaakini. *(Dora anaketi vizuri, akionekana ana hamu ya kujua zaidi)* Wewe kushika mimba inawezekana. *(Dora ana tabasamu)* Ila siwezi kukuhakikishia kama utaweza kufikisha miezi tisa bila matatizo na iwapo utafikisha, mtoto anaweza kupatikana na matatizo ya ki afya kwa ujumla.

**DORA**

Ki vipi?

**DAKTARI**

Asilimia ya wanawake ambao hupata watoto wa kiwa katika umri wa arubaini kuendelea ni 0.03, na nafasi ya mafanikio kwa matibabu ya kupunguza utasa hushuka kwa kiasi kikubwa. Kuwa na uwezo wa kupata mimba na kuendeleza ujauzito bila matatizo yoyote ni mafanikio makubwa, ukizingatia uzuri wa afya yako mwenyewe.

**DORA**

Kwa ufupi uwezekano wa mimi kupata mtoto kwa sasa ni nusu bin nusu.

**DAKTARI**

Inaweza kuhatarisha maisha yako au ya mtoto wako.

**SCENE 13**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. LOUNGE. DAY (D2)**

**<u>LEILA. SHEKUWE</u>**

SHEKUWE AMEKETI SEBULENI AKITAZAMA RUNINGA. LEILA ANASHUKA NGAZI HUKU AKIJIPODOA, HAMUONI BABAKE AKIWA SEBULENI. SHEKUWE ANAMUANGALIA. LEILA ANAREGESHA KIPODOZI CHAKE BEGINI MWAKE NA ANAPOKUWA ANATAKA KUTOKA, SHEKUWE ANAMUITA.

**SHEKUWE**

Leila, unaenda wapi saa hizi?

**LEILA**

Natoka tu kidogo baba, narudi sasa hivi!

**SHEKUWE**

Jibu swali, unaenda wapi?

**LEILA**

Town.

**SHEKUWE**

Kufanya nini?

**LEILA**

Nilikuwa nimeagana na marafiki zangu tu...

**SHEKUWE**

*(Anamkatiza)* .....huo uzembe hata mimi niliwahi kuufanya, tukiruka hapa na pale bila kujielewa. Kama sio babu yako

kunyoosha kamba, ningekuwa nimeharibikiwa na maisha haraka sana. Nitakwambia tena, achana na Beka!

**LEILA**

Aah baba nani amekwambia nae...

**SHEKUWE**

Agh! Shut up! Hivi unataka kunifanya mimi babako mpumbavu! Nipe simu yako nione kama nasema uwongo, nipe nione! *(Leila anasita, Kimya)* Mamako zako ndiyo wamefika leo, badala ya kuketi nao, wakupe mawaidha ya busara, wewe ndiyo mwanzo unataka kuzurura mitaani kutangaza ushindi!

**LEILA**

Aaah baba nimetangaza ushindi saa ngapi!

**SHEKUWE**

Unamkosea heshima mamako ASHA na kunidanganya mimi babako, kisha unajifanya uko busy hushikiki kama customer care! *(Kimya)* Nikikupata na Beka, nakuapia utatamani mimi si babako. *(Anamuacha na kuelekea juu)*

LEILA ANAKETI KOCHINI KWA HASIRA. ANAPIGA BONGO.

**SCENE 14**

**INT. LENOX'S HOUSE. LOUNGE. DAY (D2)**

**<u>DORA. LENOX</u>**

LENOX AMEANDAA MANKULI MEZANI. ANAPOSIKIA MLANGO UKIGUSWA, ANAHARAKISHA NA KUSIMAMA KANDO YA MEZA AKIELEKEA MLANGONI. ANASHIKA KITI NA KUTABASAMU, AKISUBIRI MLANGO UFUNGULIWE. DORA ANAFUNGUA MLANGO NA KUINGIA NDANI. ANAFUNGA MLANGO. ANAPOGEUKA ANAMUONA LENOX AMESIMAMA AKITABASAMU.

**LENOX**

Surprise!!

ANAMUASHIRIA VILE VYAKULA MEZANI ILA DORA HAONYESHI FURAHA YOYOTE USONI. LENOX ANAHISI KUNA JAMBO.

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**LENOX**

*(Anamfuata)* Beib nini mbaya? *(Dora anaanza kulia, anamkumbatia)* Shhh! Nyamaza, it's going to be ok! Nyamaza please! Njoo uketi, unieleze kumetokea nini!

LENOX ANAMUONGOZA DORA HADI KOCHINI. WANAKETI.

**LENOX**

Tafadhali nyamaza unieleze kumetokea nini!

**DORA**

*(Anajifuta machozi)* Nimetoka kumuona daktari, kuhusu vile tulikuwa tumezungumza!

**LENOX**

Kuhusu mtoto...Amesemaje? Haiwezekani?

**DORA**

*(Anachukua mda kusema)* Inawezekana ila daktari ameniambia inaweza kunidhuru ki afya mimi pamoja na mtoto. *(Anaanza tena kulia, Lenox anamkumbatia)* Vile nilikuwa natamani kuwa na mtoto! Inaniuma sana Lenox!

**LENOX**

*(Anamtuliza)* Usijali, afya yako kwangu ni muhimu zaidi kuliko chochote kile. Kuna watoto wengi mayatima wanaotamani wazazi kama sisi. Tunaweza ku adopt mmoja, tukampatia mapenzi yale tungeweza kumpatia mtoto wetu.

**DORA**

Kweli?

**LENOX**

Bila shaka!

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

**SCENE 15**

**EXT. SHEKUWE'S MANSION. GATE/BALCONY. DAY (D2)**

**MOMO. BE CHARO. WARIDI**

WARIDI NA BE CHARO WAMESIMAMA GETINI WAKIMUANGALIA MOMO ANAVYOPITA PITA KWENYE BALCONY. MOMO ANAWAANGALIA GHALFA, WANATAZAMA KANDO MBIO. WANAPOGEUKA HAWAMUONI.

**WARIDI**

Ametuona?

**BE CHARO**

Kukuona si hoja, hofia hizo sheria alizokuwa akitunga pale juu!

**WARIDI**

Inaonekana hanipendi?

**BE CHARO**

Hapendi yoyote, ajipenda nafsi yake mwenyewe.

**WARIDI**

Lakini wee muongo, alivyoingia umepiga vigelegele kama ambaye kumezaliwa kuku kakamega.

**BE CHARO**

Hiyo ilikuwa screensaver tu, hapa ukitaka kuishi na huyu mama ni uende anavyotaka!

**WARIDI**

©Ibrahim Chitayi © Maina Denis Wanjohi

Hilo sitofanya. Kwanza aliyeniandika kazi ni Shekuwe, hao bibi zake kila mmoja ashike adabu yake, vita vyao wapeleke kiwanjani. Kumbe hunijui. *(Anaondoka)*

**BE CHARO**

*(Anamuangalia)* Ungeniachia namba tujuane! Mmm mtoto mashallah, kiuno kama cha mchwa, ukikishika mkono haupotei, wazunguka tu kama belti! *(Acheka)*

**SCENE 16**

**INT. SHEKUWE'S MANSION. BEDROOM. DAY (D2)**

**SADA. SULTAN. MOMO**

SADA NA SULTAN WAKO CHUMBANI WAKINONG' ONEZEANA.

**SULTAN**

Maa mdogo, hapa patakalika kweli?

**SADA**

Mwanangu hapa pataka ufundi wa vitendo sio ubora wa maneno.

**SULTAN**

Mimi naona heri dada Asha atupangishie chumba tuepuke haya masaibu...

**SADA**

...hizo ni ndoto za Ali Baba kuishi majangwani na ufahari unao! Nishakwambia hapa sitoki hata pakarushwa mabomu...

MOMO ANAINGIA GHAFLA. WOTE WAWILI WANABAKI KIMYA, WAKITAHARUKI.

**MOMO**

*(Anawaangalia na kuongea nao kwa utulivu)* Nawaona mumetawala nyumba basi nahodha nisharudi, mukinileteа upuzi wenu, nitawatupa kwa maji niwazamishe. Sikuwaachilia bure, ahadi yangu lazima mtimize, nisikie tu ngwe! Mtanitambua.

ATOKA KWA VISHINDO NA KUWAACHA SADA NA SULTANA WAKIANGALIANA KWA TAHARUKI.

**©Ibrahim Chitayi** **© Maina Denis Wanjohi**

# - END OF EPISODE -

©Ibrahim Chitayi © Maina Denis Wanjohi